# KUSHUGHULIKA NA MAANDIKO YALIYOPOTOSHWA KUHUSU MUNGU NA UTAJIRI WA MALI

Pastor James Kalekwa

# KUSHUGHULIKA NA MAANDIKO YALIYOPOTOSHWA KUHUSU MUNGU NA UTAJIRI WA MALI.

James Kalekwa

# Yaliyomo

Salamu za Mama Mchungaji JK......4

Kuyafasiri Maandiko.........................6

Nguvu za Kupata Utajiri. .................9

Maskini wa roho ................................17

Kuwatumikia mabwana wawili ...22

Tajiri na masikini Lazaro................26

Maombi ya Agur bin Yake .............33

Ngamia kupenya katika tundu la sindano. ............................................ 37

Ndege wa angani............................. 44

Ya Kaisari, Tumpe Kaisari..............47

Kuhusu Mwandishi:.........................50

Kuhusu New Vine Church:............ 51

Mawasiliano na Mwandishi:.........52

# Salamu za Mama Mchungaji JK.

Juni 20, Mungu alitupa zawadi ya maisha ya mtumishi wake Pastor JK, mtu wa juhudi nyingi katika Kristo na maarifa ya kimungu. Kwa muda ambao nimekuwa naye kwenye maisha, nimemtambua kama mtu anayempenda Mungu kiasi cha mimi kukosa neno la kuelezea. Huyu ni mtu aliuzwa kwa Mungu na utumishi!

Amewekeza muda mwingi kuandika mfululizo wa vitabu hivi vya kielektroniki ili avitoe bila malipo kama sehemu yake ya ujenzi wa mwili wa Kristo… kwa niaba yake, ninaomba ukipokee kwa kuthamini dhabihu! Ninakuombea ya kwamba maisha yako yanageuzwa kwa kitabu hiki kimoja tu kwa jina la Yesu Kristo.

Pili, ninaomba uwasambazie kitabu hiki watu wengi zaidi ili maono ya kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari yatimilizwe.

Na hatimaye, kwa kuthamini zawadi ya mtu huyu wa Mungu, muombee, mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumsherehekea ukimweleza namna gani umesadika na utumishi wake – itafaa sana.

Heri ya siku ya kuzaliwa mume wangu mpenzi. Heri ya kuzaliwa Pastor JK – zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu!

Frida James Kalekwa (Mama mchungaji JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2025
Dodoma, Tanzania

## Kuyafasiri Maandiko

Kama mwanafunzi mzuri wa Maandiko Matakatifu ni vyema kuyachunguza Maandiko na kuhakikisha je, mitazamo na mapokeo yanayozungumzwa ndivyo ilivyo? Ninaandika kitabu hiki nikiwa kwenye utambuzi ya kwamba kwenye ulimwengu wa Theolojia kama taaluma huwa kuna kambi mbali mbali ambazo huyatafsiri Maandiko kulingana na kambi husika. Na imepelekea si tu kwenye taaluma bali hata kwenye utendaji (practice).

Pia ninatambua ya kwamba kumekuwa na *“extremism”* kwenye maeneo mbalimbali ya kimafundisho.

Kumekuwa na misigano ya kiuelewa/kitafsiri, kimafundisho na hivyo kupelekea misigano katika utendaji wa huduma wa siku kwa siku.

Hata hivyo, hii ndiyo imekuwa safari ya kihistoria ya kanisa (Soma historia ya kanisa). Na ndivyo kanisa limekuwa likitakaswa na kukua.

Hutokeza mkazo uliopitiliza (extreme) kuhusiana na fundisho fulani kiasi cha kupelekea upotofu; kisha hutokeza tena

kambi inayorekebisha upotofu uliotangulia… na marekebisho hayo huvutika na kuelekea kwenye upotofu mwingine.

Ili tusiendelee kuishia kuchukua maoni ya kambi hii au ile katika kukosoana na kurekebishana kwao, hebu tujiulize "Hivi ndivyo maandiko yasemavyo?"

Kwenye kitabu hiki, ninaiendea mada nyeti sana kuhusu maswala ya mali na fedha. Swali nililotamani kulijibu ni je, Mungu anahusika katika kuwafanikisha watu wake kwa mali? Na hapa nimejielekeza kushughulika na Maandiko pendekezwa ambayo hutumika kutibu

*“extreme”* ya kile kiitwacho *“Injili ya Mafanikio.*

Katika safari hii, tutayahoji Maandiko Matakatifu tu bila kuingiza maoni ya kambi yoyote ya kitheolojia. Biblia ijieleze yenyewe!

## Nguvu za Kupata Utajiri.

Ni jambo la maana sana unaposoma Biblia na kuelewa kwa mapana nini mwandishi amekusudia katika kila neno

*Kumbukumbu la torati 8:18SUV "Bali utamkumbuka Bwana, Mungu wako, maana ndiye akupaye nguvu za kupata*

*utajiri; ili alifanye imara agano lake alilowapa baba zako, kama hivi leo."*

Biblia inatuelezea utajiri sio jambo linalojitokeza tu bali utajiri hupatikana kwa nguvu.

Ningeweza kuwekeza mjadala mrefu kwenye andiko hili kulihoji lijitafiri jenyewe. Kwa mfano, ili tuweze kuwa kwenye uelewa mmoja ni lazima tufikie hitimisho moja ya kwamba kwa neno “utajiri” kwenye Maandiko haya ni nini hasa kinachorejelewa.

- Kula na kushiba (mstari 10,12)

- Kujenga nyumba nzuri na kuishi ndani yake (mstari 12)
- Kuwa na maongezeko ya mifugo (mstari 13)
- Kuwa na maongezeko ya fedha na dhahabu (mstari 13)
- Kuwa na maongezeko ya kila kitu (mstari 13)

Hayo ndiyo maneno halisi yanayotumiwa na Biblia. Si vyema kuanza kurohosha kama vile hayo yaiyotajwa si mambo ya kiroho.

Sasa, kuna onyo linafuatia baada tu ya hayo:

Kumbu. 8:17, *“Hapo usiseme moyoni mwako, Nguvu zangu na uwezo wa mkono wangu ndio* ***ulionipatia utajiri huo.****”*. Hili neno “Utajiri huo” linaonyesha ya kwamba muwasilishaji wa ujumbe na hadhira ya ujumbe wana uelewa unaofanana kuhusiana na utajiri. Anautaja kama vile kuuelekezea kidole “Huo!”. Kwa msomaji makini wa Biblia, atakubaliana mimi kwamba kama ni “utajiri huo”, basi uko kwenye mistari hiyo hiyo… uko tu karibu!

Sasa, Biblia inatoa onyo kwa wana wa Israeli ya kwamba baada ya hayo kutokea; ambayo ndiyo tafsiri ya utajiri, mioyo yao

isiinuke na kujisema kuwa wao ndiyo chanzo cha utajiri. Maana yake inawezekana kuwa hivyo! Halafu hitimisho ni kwamba, wanapaswa kumkumbuka Bwana kwa kuwa ndiye awapaye **nguvu za kupata utajiri!**
Ndiyo ni nguvu… halafu ni nguvu iliyoelekezwa kwenye jambo fulani mahususi – kupata utajiri! Kuna kificho hapo?

Kuna mambo kadhaa katika Biblia yaliolezewa kuwa yanapatikana kwa nguvu; na mojawapo ni utajiri!

Kama ni hivyo basi, adui shetani pia anatamani kuona watu wakielewa vibaya kuhusiana na jambo hili. Na uelewa mbaya huzalisha kuamini vibaya na kupelekea utendaji mbaya!

Kwa sababu matokeo ya kuelewa vibaya jambo hili huleta matokeo hasi ambayo kwa mantiki ya Maandiko ni kwamba utajiri unaweza kuhamisha moyo wa mwanadamu na kumpelekea kumsahau Mungu – ndivyo Maandiko yanavyosema!

Kutokea kwenye dhana ya imani kuwa ndiyo mwamuzi wa maisha yote ya mwamini, basi ukielewa jambo lolote vibaya lazima utaenenda vibaya. Uelewa

wako kuhusu Mungu na neno lake huamua mifumo yote ya maisha yako ienende kwa namna gani. Huwa inapenda kusema, *"Theolojia (Elimu yako kumuhusu Mungu) yako huamua olojia (elimu nyinginezo) zako zingine!"*

Kama si Mungu awapaye watu wake nguvu za kupata utajiri (tafadhali rejelea maana ya utajiri kwa muktadha wa andiko hili), basi itakuhangaisha sana ukijikuta una maongezeko… utaona adui ameingia kukufanikisha, utakemea badala ya kushangilia na kumtukuza Mungu. Tena, hutaweza hata kuamini achilia mbali

kuomba kwa ajili ya utajiri huo ambao Mungu hutoa nguvu kuupata.

Katika kitabu hiki tutajikita katika kufahamu mambo gani ambayo yamepelekea waamini kuona ni kawaida kuwa maskini na kubaki katika mgongo ya kwamba ni neno la Mungu ndiyo limesema haya. Nitakuongoza kwenye kufikia hitiisho ya kwamba huo ni uelewa mbaya. Maandiko mengi yanayorejelewa, yametafsiriwa kulingana na kambi ya kitheolojia. Hebu tuyahoji leo na yazungumze nasi.

Roho Mtakatifu akupe utulivu na nafsi, unyoofu wa nia, utiifu moyoni na mwitikio stahiki kwenye kila Andiko!

Ifuatayo ni misamiati au sehemu ya Neno kutoka katika biblia ambayo wakristo wa leo wameielewa vibaya kuhusu Mungu mali na vitu**.**

## Maskini wa roho

*Mathayo 5:3SUV "Heri walio maskini wa roho; Maana ufalme wa mbinguni ni wao."*

Hii ni sehemu ya kile kinachofahamika kama "Hotuba ya Mlimani!" kwenye injili ya Mathayo. Kwa ufupi, injili ya Mathayo

inamtambulisha Bwana Yesu kama Mfalme wa Israeli – Mwana wa Daudi (Mfalme ambaye aliambiwa uzao wake utakuwa na enzi ya milele); mwana wa Ibrahimu (baba ambaye aliambiwa kwa uzao wake mataiafa watajibarikia). (Mathayo 1:1).

Sasa, mistari inayofuata hapo inafuatilizia kumpata “mwana wa ahadi” na “mfalme mwenye enzi isiyo na mwisho”. Simulizi yote inakuja kugota kwenye kuzaliwa kwake Yesu Kristo. Kisha inaenda kuonyesha hamaki inayozaliwa nyumbani kwa Herode – mtawala wa kisiasa!

Kuna mengi tungeweza kuyaendea kwa kina, lakini ni vyema ufahamu, Mfalme Yesu Kristo anatangaza ufalme wake na sheria zake mpya na bora zaidi. Anahamisha sheria kutoka mwilini kwenda rohoni… ndipo anaposema *“Heri masikini war oho…”*

Wakristo wengi wametumia andiko hili vibaya ya kwamba, *“tuna heri sisi tulio masikini maana ufalme wa mbinguni ni wetu.”*

Kwa wengi, umasikini umeambatanishwa na uheri, kwa uelewa wao kuhusiana na andiko hilo.

Mpendwa wangu ni kweli unaweza kuwa masikini wa vitu (material things) na ukaingia katika raha ya ufalme wa mbinguni na vilevile unaweza kuwa tajiri na ukaingia katika raha ya ufalme wa mbinguni.  Biblia haijasema masikini wa vitu ndio ufalme wa mbingu ni wao Hapana! Kimsingi, Biblia haijaishia kusema masikini… imesema masikini wa roho… na haijasema masikini wa mali ndiye mwenye heri!

Tunaposema maskini tunamaanisha nini mchungaji? Unaweza kuhoji…

- ✓ maskini ni mtu asiye na kipato cha kujikimu.

- ✓ ni mtu asiyeweza kulipia gharama zake mwenyewe yaani ni muhitaji.
- ✓ ni mtu anayehitaji mtu mwingine aingilie kati kwenye maisha yake.

Kutokea kwenye kitabu cha injili ya Mathayo Mtakatifu anasema heri (yaani wamebarikiwa) , hao walio masikini wa roho! Hii ina maanisha hao ambao ni wahitaji wa kiroho, hwawejiwezi kiroho, wanahitaji mtu mwingine aingilie kati kwenye hali yao ya kiroho… wanamuhitaji Bwana Yesu ayafanikishe maisha yako. Hawa ni watu ambao utoshelevu wao ni ufalme wa Mungu.

Kwahiyo, tunaposoma na kulichambua neno la Mungu, hamaanisha masikini wa vitu ndio watakaorithi ufalme wa Mungu bali hao walio na uhitaji na Yesu kwenye maisha yako ili kusudi watoshelezwe naye!

Kwa mujibu wa andiko hili, uheri ni uhitaji wa kiroho… kumuhitaji Bwana Yesu na ufalme wake!

## Kuwatumikia mabwana wawili

Hii pia imekua methali ya wakristo wengi wakiamini kwamba watu wote wenye mali hawawezi kumtumikia

Mungu…kumuishia Mungu, kumwelekea Mungu! Kwani haiwezekani kutumikia mabwana wawili.

Ni sahihi kabisa ya kwamba haiwezekani kuwatumikia mabwana wawili kwasababu utampenda mmoja na kumchukia mwingine. Biblia inasema hivi Mathayo *6:24 "Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali."*

Ubwana ni nini? ni hali ya umiliki; hali ya kuwa na utawala na kuwa na mamlaka kuu

kwenye maisha ya mtu na mambo yote yanayohusiana na yeye!

Ubwana umegawanyika katika maeneo mawili ambayo ni;

a) Ubwana wa lazima (yaani hapa mtu hutumikishwa pasipo hiari – huburuzwa tu)
b) Ubwana wa hiari (hapa ni mtumwa hutumikia kwa hiari yake mwenyewe)

Kimsingi, kinachozungumzwa kwenye andiko hili ni kujisalimisha kikamilifu (total surrender) kwenye ubwana wa Yesu Kristo. Yaani, mimi na kila

kinachohusiana na maisha yangu. Yesu hawi Bwana kamili kwenye maisha yangu iwapo kuna vipande sijavisalimisha kwake… nitakuwa ninatumikia bwana mwingine! Nimewahi kusema jambo hili ya kuwa *"Iwapo Yesu si Bwana wa yote basi si Bwana kabisa..."*. Yesu hataki kuwa Bwana kidogo… anataka kuwa Bwana kikamilifu!

Kwa hiyo, anachokitafuta ni “mimi na mali” kujisalimisha chini ya ubwana wake! Na hapo ndipo unaweza ukaelewa vyema ya kwamba anataka kuwa Bwana wa mali alizonibariki nazo.

Kwa kuwa kinachotafutwa ni moyo uliosalimishwa kikamilifu ili mimi mtumwa wa Bwana nitumike na mali chini ya Bwana au nimtumikie Bwana kwa mali kwasababu mali ni mtumwa mzuri ila ni bwana mbaya.

## Tajiri na masikini Lazaro

*Luka 16:19-21SUV "Akasema, Palikuwa na mtu mmoja, tajiri, aliyevaa nguo za rangi ya zambarau na kitani safi, na kula sikuzote kwa anasa. Na maskini mmoja, jina lake Lazaro, huwekwa mlangoni pake, ana vidonda vingi, naye alikuwa akitamani kushibishwa kwa makombo yaliyoanguka katika meza ya yule tajiri;*

*hata mbwa wakaja wakamramba vidonda vyake*."

Ili uweze kufurahia uzuri wa habari hii, ni vyema ukaelewa mtindo wa mafundisho na uwasilishaji wa Bwana Yesu.

Kwenye mifano yote ambayo Yesu alifundisha hakuwahi kutaja jina la mtu kimahususi kwenye simulizi… Mara zote amekuwa akisema "Mtu mmoja…", "Kabaila mmoja…". Mifano yote ya Bwana Ysu haikuwa na majina ya watu.

Kwa hivyo, kwa msomaji makinifu wa Maandiko anapokutakana na muundo (pattern) tofauti wa uwasilishaji wa

fundisho, ni lazima afungue masikio yake kwa nguvu kutaka kuelewa kinachosemwa.

Biblia inaelezea habari ya watu wawili masikini na tajiri. Tajiri hatambulishwi kwa majina yake bali kwa mavazi, chakula na mtindo wa maisha yake! Na inaendelea mbele inasema kwamba tajiri alikua akila vizuri katika hali ya anasa. Hali ya anasa ni nini?

- ✓ Kutojali: n*i kufanya mambo kama vile wewe ndio chanzo cha mambo hayo na chanzo chako wewe mwenyewe.*

- ✓ Kutotambua mipaka yako: *ni kusema hakuna Mungu*.
- ✓ Kutowajibika popote: *ni kusema hakuna mamlaka ya juu inayokuwajibisha*.

Hii habari ya watu wawili inaelezea namna tajiri alivyotumia mali zake kwa anasa – ***siku zote!***

Hili halikuwa tukio la bahati mbaya, au kupitia, kujisahau au kushawishiwa. Hii inaonekana ni jambo lilalofanywa kwa kujua na kukusudiwa. Huu ndiyo mtindo wa maisha yake na mwenendo wake kwa ujumla.

Kosa la tajiri ni kutumia kwa *anasa siku zote!* Hakukuwa na ubaya kama angechagua kutumia mali kwa utukufu wa Mungu siku zote! Yaani alipaswa azitumie fedha zake na mali zake. Swala ni namna gani alitumia ndipo palikuwa na shida yake.

Hili unaliona vizuri unapomleta Lazaro kwenye simulizi kwa namna ya kumlinganisha (contrast) na tajiri. Lengo la fundisho hili la Bwana Yesu ni kuchora hali ya ulingani baina ya wahusika hawa wawili!

Waamini wengi wa leo wanaona ni nzuri kuwa kama maskini Lazaro ili waingie

ufalme wa mbinguni.  Hata hivyo, Lazaro kwenye habari hii ni zaidi ya jina tu. Kwa nini tupewe jina la huyu wakati hatujapewa jina la tajiri? Jina la Lazaro linafanya nini kwenye mfano huu wakati mifano mingine mahala pengine kwenye mafundisho ya Bwana Yesu haitaji majina ya watu? –Inatafakarisha!

Kumbe Lazaro hapa ni jina na ni hali ya moyo. Jina hili limetokana na neno la kiebrania linaloitwa El - azar maana yake Mungu ndiye msaada wangu; ndiye anisaidieaye/Mungu amesaidia.

Kwa hiyo, Lazaro, kwenye simulizi hii inaonyesha tumaini la masikini huyu

lilikuwa ni nani? – Mungu. Ukilinganisha sasa na tajiri aliyekuwa akila na kuvaa siku zote kwa anasa, utaona tumaini lake lilikuwa ni mali!

Kosa la tajiri halikuwa utajiri. Uheri wa Lazaro haukuwa umasikini. Bali, tajiri alikuwa anaishi kwa anasa siku zote (tumaini lake ni yeye mwenyewe na mali zake) wakati Lazaro, tumaini lake lilikuwa kwa Bwana.

Kumbe inawezekana pia kuwa tajiri Lazaro!

# Maombi ya Agur bin Yake

*Mithali 30: 7-9 "Mambo haya mawili nimekuomba; Usininyime [matatu] kabla sijafa. Uniondolee ubatili na uongo; Usinipe umaskini wala utajiri; Unilishe chakula kilicho kadiri yangu. Nisije nikashiba nikakukana, Nikasema, Bwana ni nani? Wala nisiwe maskini sana nikaiba, Na kulitaja bure jina la Mungu wangu*."

Maombi haya ya Agur yametumiwa na wengi kwenda extreme ya kuonyesha ni uovu mwingi kiasi gani unaletwa na kuwa

na mali nyingi! Hii ni kweli… LAKINI ni kweli nusu.

Kwenye haya maombi ya Agur mwana wa Yake, ameonesha ya kwamba nikiwa tajiri sana, ninaweza kukukana hadharani lakini pia nikiwa maskini nitakukufuru wewe Mungu. Imeonyesha tabia mbili za kundi la utajiri na umasikini.

Utajiri – unaweza kumwingiza mtu kwenye sanduku la kumsahau Mungu.

Umasikini – unaweza kumfanya mtu kumfukuru Mungu.

Na wakristo wengi wamejificha katika ombi na kuutukuza umaskini katikati yao.

Lakini Agur, kiuhalisia aliona hatari za mambo yote mawili, yaani utajiri na umasikini. Ndiyo maana hakuuomba umasikini kama tu ambavyo wanaoupinga utajiri hawawezi kuthubutu kufungua vinywa vyao kuomba umasikini!

Kimsingi, Agur anaomba hili hali akiangalia uwezo wa moyo wake kubeba. Amejitambua hawezi kubeba umasikini sana na vilevile hawezi kubeba utajiri sana.

Huwa ninawaambia watu, kama moyo wako unaweza ukabeba swala la shibe na uwingi, basi unaweza kuendelea mbele na njia ya utajiri. Pia, moyo wako kama

unaweza kutosheka na hali ya umasikini na uhitaji kiasi cha kutovutiwa kuiba au kulikufuru jina la Mungu, basi endelea mbele kwenye njia ya umasikini.

Hekima za Agur zinatuonyesha ya kwamba iwe ni umasikini au utajiri, kila kimoja huja na changamoto zake. Ni wewe tu kuchagua ni changamoto gani ungependa kushughulika nazo.

Kiini cha ombi hili ni kutambua hali ya moyo wako na nini hali hizi mbili zinaweza kufanya na moyo wako!

Nimechagua kuwa tajiri, ninayeshiba na kuwa na mazidisho kisha kumuheshimu Mungu kuwa ndiye asili ya baraka zote.

Kwamba Agur aliomba umasikini? Kwamba Agur aliukemea utajiri? HAPANA!

## Ngamia kupenya katika tundu la sindano.

*Mathayo 19:23 -26SUV "Yesu akawaambia wanafunzi wake, Amin, nawaambieni, ya kwamba itakuwa shida tajiri kuingia katika ufalme wa mbinguni. Nawaambia tena, Ni rahisi zaidi ngamia kupenya tundu ya sindano, kuliko tajiri*

*kuingia katika ufalme wa Mungu. Wanafunzi waliposikia, walishangaa mno, wakisema, Ni nani basi awezaye kuokoka? Yesu akawakazia macho, akawaambia, Kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu yote yawezekana.".*

Ukisoma andiko hilo pia kwenye tafsiri nyingine na lugha za asilia kisha ukawekeza muda kuelewa historian a muktadha, inakuwa kazi rahisi sana kuyatafsiri yanayozungumzwa.

Hebu tazama hapa:

Luke 10:25, *"It is easier for a camel to go through the eye of a needle than for a rich man* ***[who places his faith in wealth or status]*** *to enter the kingdom of God."*

Kwenye jamii ya Kiyahudi ya wakati huo, walibeba uelewa wa ahadi ya baraka za Bwana kwa baba Ibrahimu kuhusu utele na utajiri kiasi cha kuweka utajiri kama kipimo cha ukiroho wa watu. Ndiyo maana moja ya jambo ambalo Bwana Yesu alikuja kulisawazisha ni kutoa mizani ya ukiroho kwenye umiliki wa mali. Ni changamoto ambayo hata sasa inapenya ndani ya kanisa.

Si unafahamu ni kwa bidii kiasi gani Bwana Yesu aliikuta jamii ya kiyahudi ikitafuta utajiri na vyeo vya hadhi na kuonekana? Kwa sababu, ndiyo vilikuwa vipimo vya ukiroho vya wakati huo.

Kinachosemwa kwenye andiko hili ni jitihada ya tajiri kuungia ufalme wa Mungu kwa kutumia kigezo cha mali na utajiri wake.

Kwa upande mwingine, kuna hiki kinachoitwa “tundu la Sindano”. Huu ulikuwa ni mlango mdogo wa kuingilia kwenye mji (ieleweke ya kwamba miji ilikuwa inazungukwa na kuta kama vile ukuta wa Yeriko!). Sasa, lango kuu

ambalo lilikuwa linaweza kuingiliwa na kila mtu na kila aina ya mnyama, lilikuwa likifungwa. Kulikuwa na kamlango kadogo kalikofahamika kama tundu la sindano… ambapo, mtu ingemlazimu kumuacha ngamia wake nje ya lango na apakue mzigo wake na kuuingiza kidogo kidogo, kisha ngamia aingia kwa kujikunja sana.

Kwa ulinganifu huo, Bwana Yesu anaonyesha inawezekana ngamia kupenya kuliko tajiri akijaribu kuingia kwa kutumia mali zake mwenyewe.

Unaelewa ya kwamba ilimbidi ngamia ashushe mizigo yote ndiyo aweze kupenya

kwenye tundu la sindano? Sasa, ndicho anachofundishwa tajiri… kushusha mizigo yake… kuondoa matumaini yake juu ya mali!

Kumbe anachokisema Bwana Yes si kwamba matajiri hawatakiwi kuingia LAKINI anachowasilisha ni wanaingiaje!

Hivi umesoma mwitikio wa wanafunzi wa Yesu baada ya fundisho hilo: ***Ni nani basi awezaye kukoka?*** Hiyo ni kuonyesha na wao walikuwa ni matajiri na mambo yamekuwa magumu.

Ninafurahia jibu la Bwana wangu Yesu Krsito: "*Yesu akawakazia macho,*

*akawaambia,* ***Kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu yote yawezekana.***" Hili andiko la kwa Mungu yote yanawezekana, tumelitumia sana kwa ajili ya maombezi na kufunguliwa. Hata hivyo, muktadha wake ni tajiri kuuingia ufalme wa Mungu.

Hitimisho ni kwamba kumbe kwa Mungu inawezekana tajiri kuuingia ufalme wa Mungu!

Mwanadamu kwa bidii yake mwenyewe kamwe hawezi kuingia ufalme wa mbinguni. Na hiyo ni kuwapa mualiko ya kwamba kila mmoja ni masikini yaani

muhitaji kiroho na mtegemezi kwa Mungu pekee yake ili aione mbingu.

## Ndege wa angani

*Mathayo 6 :26SUV "Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je! Si bora kupita hao?"*

Kuna jamii ya waamini wamejificha katika huu mstari ya kwamba; maua yanavishwa na ndege wa angani wanakula

na hawapandi. Hakuna kitu wanachokifanya bali Mungu anajishughulisha na maisha yao kwa asilimia zote.

Kwa hiyo hitimisho la jamii ya waamini inayotafsiri nadiko hili hivyo, huamini ya kwamba na sisi ndivyo ambavyo Mungu atafanya kwetu. Tutakaa na kujiachia hali tukisubiri kulishwa kama ndege au kuvishwa kama maua ya kondeni.

Ni sahihi kabisa Mungu atakulisha ewe mwanadamu; walakini kwa kila kiumbe Mungu amekiandalia mchakato (mechanism) wake wa upaji wa kiungu. Katika mchakato wa kiungu kwa

mwanadamu, ameandaa mfumo wa kuyapendezesha maisha yake kwa baraka. Na ndiyo maana anasema atabariki kazi ya mikono... hiyo ni kutuambia kwamba mwanadamu fanya kazi na Mungu atakubarikia; na tuache kukaa kama sisi ni ndege kwasababu mfumo wao wa upaji ni tofauti na upaji wa mwanadamu. Tunaweza kujifunza kwa utegemezi wa ndege kwa Mungu; twaweza kutazama upaji wa Mungu katika kuyapendezesha maua. Hata hivyo, sisi si ndege wala maua… kuna mfumo wa upaji wa Mungu kwa wanadamu. Huo umo katika kufanya kazi kwa lengo la kuzalisha matokeo yanayomtukuza Mungu!

## Ya Kaisari, Tumpe Kaisari.

*Marko 12 :17SUV " Yesu akajibu, akawaambia, Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na yaliyo ya Mungu mpeni Mungu. Wakamstaajabia sana*."

Hili ni andiko ambalo hurushwa huku na kule na wasiojua kabisa neno la Mungu. Humaanisha mambo ya kujipatia utajiri (au mambo yoyote yanayohusisha kazi za mikono, uzalishaji mali) ndiyo mambo “Ya Kaisari!”. Watu wa namna hii hujaribu kutenganisha baina ya mambo ya kiroho (mambo ya kikristo) na mambo ya Kaisari.

Hii imepelekea uvivu au kuchukua hatua hafifu sana kuyaelekea mambo ya utajiri wa mali na ustawi.

Ni rahisi sana, kusanyiko lilimuhoji sana uhalali wa kulipa kodi kwa Kaisari (ukisoma andiko lote kwa ujumla)

Yesu akawambia makutano ya kwamba kwasababu dinari (kama vile shilingi kwenye mazingira yetu ya kitanzania) ina picha ya Kaisari basi mpeni Kaisari – yaani alipwe kodi kutumia fedha yenye taswira yake! na yaliyo ya Mungu mpeni Mungu.

Hapa mkazo wa andiko uko hivi: Kama fedha ndiyo ina picha ya Kaisari, je picha ya Mungu iko kwa nani? Au kwenye nini? – Ipo kwa wanadamu; tumeumbwa kwa sura na mfano wa Mungu.

Kwa bahati mbaya sana Kaisari hupewa vya Mungu! Wewe ni mali ya Mungu. Nafsi yako ni mali ya Mungu. Unajali sana fedha yako inaenda wapi (kwa Kaisari au kwa Mungu) na kutojali sana wewe unaenda wapi?

**Kuhusu Mwandishi:**

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor, Priscilla na Butogwa; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: Pastor James Kalekwa

Instagram: @pastorjameskalekwa

Youtube: Pastor James Kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

**NEW VINE CHURCH** | **Dodoma**



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

**Ratiba za Ibada**

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni

**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor ,Priscilla na Butogwa. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
MchungajiJK
jameskalekwa.com
+255 754 917 764
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
+255 754 917 764